**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI IBWAGA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**
**Mkuu wa Shule: 0717 246420**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0654 811019**
**Matron: 0713 903833**

**Shule ya Sekondari Ibwaga, S.L.P 31,**
**Kongwa.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………**
**……………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI IBWAGA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA MKOA WA DODOMA MWAKA ..............................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ................... na atasoma tahasusi ya ...............

Shule ya sekondari Ibwaga ipo umbali wa kilomita 7 mashariki mwa mji wa kongwa. Usafiri wa basi kutoka Dodoma mjini unapatikana katika kituo cha mabasi JOB NDUGAI (NANENANE) na nauli ni shilingi Elfu 5,000/= (kwa gari zinazofika Kongwa) na 7,000/= (Kwa gari zinazofika mpaka Ibwaga) Ukitokea Dar es salaam kuna mabasi yanayoelekea **MPWAPWA** kupitia **KONGWA** au ukipanda mabasi yanayoelekea Dodoma kutoka Dar es salaam shukia kituo cha **MBANDE** kuna bajaji za kuelekea Kongwa mjini nauli ni shilling 2,000/=. Kutoka stendi ya Kongwa kuna bodaboda za kuelekea shuleni na nauli ni shillingi 4,000/=, na bajai nauli ni shilingi 10,000/=

Muhula wa Masomo unaanza tareh ................, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ...........................

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia: - SARE YA SHULE:

**a) Kwa wasio waislamu:**

- Mashati mawili (02) meupe ya mikono mirefu na mfuko upande wa kushoto.
- Sketi mbili (02) za drafti zenye rangi nyeusi, damu ya mzee na nyeupe. Mshono wa rinda mbili (2) ndogo kila upande kulia na kushoto na kubwa moja mbele na nyuma, iwe ndefu ivuke magoti kama inavyoonekana kwenye picha hapo chini.




- Kwa atakayekwama kupata kitambaa, sketi hizi pia zinapatikana Ibwaga kwa gharama ya Tsh. 26,000.00

**b) Kwa waislamu:**

- Hijabu (Juba) nyeupe isiyo na urembo na iwe ndefu kufunika mikono.
- Nusu kanzu ndefu mpaka usawa magoti
- Suruali pana ya kitambaa cha drafti yenye rangi nyeusi, damu ya mzee na nyeupe kama inavyoonekana hapo chini.



- Kwa atakayekwama kupata kitambaa, nguo hizi pia zinapatikana Ibwaga kwa gharama ya Tsh. 26,000.00

c) Sare za michezo kwa shule hii ni **track suit dark blue** yenye mistari meupe mitatu pembeni (isiyo na kofia ya kufunika kichwa) na raba nyeusi.

d) Viatu vya shule vyeusi vya ngozi vyenye kamba na vyenye visigino vifupi

e) Soksi (stocking) nyeupe jozi mbili ndefu kama zinavyoonekana kwenye picha hapo juu.

f) Nguo za kushindia:

- Gauni (shamba dress) mshono wa solo iwe ndefu mpaka kwenye vifundo vya miguu, kitambaa (aina ya polista/ tetroni) cha drafti ndogo za rangi nyeupe na blue bahari kama inavyoonekana kwenye picha.



- T shirt mbili (Form six), rangi ya kijivu yenye kola nyeusi yenye ufito mweupe kama inavyoonekana kwenye picha.

.

- Masweta Mawili rangi ya kijani (dark green) shingo V.

## 2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -

i. Ream ya karatasi nyeupe aina ya A4 mbili (02) kwa mwaka.

ii. Picha 2 za passports size (background ya rangi ya bluu).

iii. Mwanafunzi anatakiwa kuja na vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

iv. Dissecting kit na Scientific calculatorkwa wanafunzi wa CBG.

v. Godoro la futi 2.5 x 6

vi. Mashuka jozi 2 (pink), Blanketi 1, Chandarua 1 chenye ukubwa wa futi 3 au 4 ya square ambayo ni nyeupe, taulo na jozi moja ya kanga au kitenge. (Nguo nyingine zisizo sare ya shule hazitakiwi) vii.Vyombo vya chakula: (Sahani, Bakuli na kikombe visiwe vya plastiki, kijiko na chombo safi cha kuhifadhia maji ya kunywa (Galoni ya lita tano kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa). viii.Mwamvuli.

ix. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.

x. Kwanja 1, jembe 1 lenye mpini, mifagio ya ndani na nje (Soft boom na ufagio aina ya chelewa kwa tahasusi (combination) ya HKL na (Hardboom na Hadimopa, reki 1, kwa tahasusi (combination) ya CBG.

xi. Aje na Sabuni za kuogea na kufulia, mswaki na dawa ya meno, mafuta ya kupaka, losheni, pedi za kike, skini taiti, Brazia iwe nyeupe au nyeusi pia aje na chupi za kutosha (zisipungue tano).

xii. Sanduku la chuma (tracker), na Torch.

xiii. Ndala za kuogea (kandambili)

**Vifaa vya darasani: Madaftari makubwa 12 (Quire 3 au 4), Daftari ndogo (msomi) za kutosha kulingana na tahasusi yake, Rula 1, Kalamu za kutosha, Penseli na Mfuto, Begi zuri jeusi la kubebea madaftari na vitabu, Mathematics set 1.**

## 2.2 Michango mbalimbali

### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **IBWAGA SECONDARY SCHOOL CAPITATION GRANTAKAUNTI Na.50301200044** katika bank ya NMB. (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay slip na Tahasusi /combination yake)

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation); iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule; vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa; viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- ❖ **Mawasiliano na taarifa yoyote ipitie kwa uongozi wa shule.**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

   i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
   ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
   iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
   iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shue 0717 246420/0611113653**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0654 811019**
- **Mwandamizi Taaluma 0717426276**
- **Mwandamizi Malezi 0713 903833**

**KARIBU SANA IBWAGA SEKONDARI**

**...........................**

**EVA A. MWANSILILO MKUU WA SHULE**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a Medical Officer from a known public hospital/ health Centre in respect to all entrants.

Full name: ………………… age: … Sex: …… year: ……

1. Blood Count (Red and White): ……………………………………………………
2. Urine analysis Test: ……………………………………………………………
3. Syphilis Test: ……………………………………………………………………
4. T.B. Test: …………………………………………………………………………
5. Eye Test: …………………………………………………………………………
6. Ears: ………………………………………………………………………………
7. Spleen: ……………………………………………………………………………
8. Abdomen: …………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION:**

EG: Physical defects or impairment(S) infections chronic or family diseases, etc.

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………

**…………………………………….** **……………………………………**

**NAME AND DESIGNATION** **SIGNATURE AND OFFICIAL STAMP**

**……………………………………** **……………………………………..**

**STATION** **DATE**

**NOTE:**

Medical Officer during the course of this examination, please attend the individual according to any diagnosed case

**NB:**

This form should be sent to school with acceptance form or brought when you come to school. No student will be enrolled without certification of physical fitness.

**OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI IBWAGA**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI NA AHADI**

**A. KIAPO CHA MWANAFUNZI (IJAZWE NA MWANAFUNZI)**

1. JINA KAMILI …………………………………………………..
2. UMRI ………………………………………………………….
3. TAREHE YA KUZALIWA …………………………….
4. MKOA ALIPOZALIWA ………………………………..
5. WILAYA ALIPOZALIWA ……………………………..
6. KABILA LAKE …………………………………………

Mimi …………………………………. Mwanafunzi wa kidato cha tano nimesoma na kuzielewa sheria za shule, naahidi kuwa nitazitekeleza kadri ya uwezo wangu. Nikishindwa kuzitekeleza hatua zichukuliwe na uongozi wa shule kulingana na kosa dhidi yangu. Hii ni pamoja na kusimamishwa au kufukuzwa shule. Pamoja na haya yote nitajitahidi zaidi kuhakikisha kwamba wastani wangu kitaaluma ni mzuri.

SAHIHI YA MWANAFUNZI …………………………….. TAREHE ………………………..

**B. KIAPO CHA MZAZI (IJAZWE NA MZAZI**

1. JINA KAMILI …………………………………………
2. MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ………………………
3. UHUSIANO NA MWANAFUNZI ……………………………
4. KAZI YANGU NI ……………………………………………
5. ANUANI/MAHALI NINAPOTOKA ………………………
6. NAMBA YA SIMU ………………………………………… (Unaruhusiwa kuweka namba zaidi ya moja)

**PICHA YA MZAZI**

Mimi …………………….…. Mzazi/mlezi ninakubali mtoto wangu ……………………… asome katika shule ya Sekondari Ibwaga tangu tarehe ……………… Naahidi kwamba: -

a) Ninakubali kumpatia vifaa vilivyotajwa katika orodha na kuwa nitamhimiza mtoto wangu afanye bidii na kutii sheria za shule.
b) Naelewa kuwa nafasi hii ya wito wangu kuingia kidato cha tano siyo haki yake ila ni bahati aliyotunukiwa na Taifa. Naahidi ya kuwa nitahakikisha anafuata sheria za shule ashindwapo hatua zozote zichukuliwe dhidi yake.
c) Nimekubali tahasusi aliyopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI ............................................... TAREHE..........................